


Kwa maelezo zaidi wasiliana na TORITA:

S.L.P. 431, Tabora , Simu/Fax

+255 732 988 245

Barua pepe: info@torita.or.tz

Tovuti: www.torita.or.tz

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA**

**TAASISI YA UTAFITI WA TUMBAKU TANZANIA (TORITA)**

# BAMETHIRIN 2.5 EC



# BAMETHRIN 2.5EC

## 1.0 Utangulizi

Uzalishaji wa tumbaku hapa nchini unategemea sana madawa ili kudhibiti wadudu mbalimbali ambao hushambulia tumbaku. Bila udhibiti wowote hasara katika uzalishaji wa tumbaku inaweza kufika asilimia 100.

Bamethrin 2.5 EC – ni kiuadudu cha kuangamiza wadudu mbali-mbali kama vimatira, vidomozi, funza wa vitumba kwenye zao la tumbaku.

**2.0 Viwango vya viuatilifu:**

Deltamethrin 25g/l

**3.0 Wadudu wanaodhibitiwa:**

Chawa wa majani, funza wa vikonyo na inzi weupe.

**4.0 Jinsi ya kutumia**

i. Pima kiasi cha mililita 8 za dawa ya bamethrin 2.5EC changanya na maji lita kumi, na tikisa vizuri ili dawa ichanganyike na maji vizuri.

ii. Tumia mchanganyiko huu siku hiyo hiyo

iii. Yaweza kupuliziwa kwa kutumia kifaa chochote, haina madhara kwa chombo (ndege, trekta).

**5.0. Muda wa kuweka:**

Baada ya wadudu kuonekana

**Angalizo:**

1. Tumia maji safi.
2. Tumia vifaa vya kukinga mwili wakati wa kutumia.
3. Dawa itunzwe stoo kwenye hali ya ubaridi na ukavu pia weka mbali na watoto
4. Dawa itumike wakati wa asubuhi au jioni ilikuepuka athari zinazoweza kusababishwa na jua kama vile kupotea kwa dawa kwa njia ya mvuke (Evaporation)